#WeweNdoFuture #TimizaWajibu

# HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo Na. 17 Jan - Machi 2025

## JAMBO LETU



Jacqueline Msuya
*Mhariri*

# WAZIRI MKUU MAJALIWA AHITIMISHA MAADHIMISHO YA MIAKA 20 YA HESLB



## *Abainisha wanafunzi 830,000 kunufaika mikopo yenye thamani ya TZS 8.2 trilioni*

***Dar es salaam, Februari 17, 2025***

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB) amemwakilisha Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye kilele cha maadhimisho ya miaka 20 ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) yaliyofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Katika hotuba yake, Mhe. Majaliwa amesisitiza kuhusu HESLB kuboresha mahusiano zaidi na taasisi za kifedha ili kuongeza ufanisi na kutoa elimu ya kutosha kwenye shule za sekondari zenye kidato cha tano na sita kuhusu sifa, vigezo na taratibu za utoaji wa mikopo hii kwa wanafunzi wanaotarajia kujiunga na vyuo vikuu na vya kati nchini.

"Naishauri Bodi ya Mikopo ikae pamoja na taasisi za kifedha ili kuangalia namna nzuri ya kushirikiana na kuwezesha watanzania wengi kusoma elimu ya juu…lakini vilevile elimu kuhusu mikopo itolewe kwa wanafunzi wa sekondari ambao hao ndio haswa walengwa wa mikopo hii ya elimu ya juu", amesema Mhe. Majaliwa.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu ambaye pia ni mnufaika wa mikopo ya elimu ya juu, amewashukuru na kuwapongeza viongozi watangulizi wake walioona mbali na kuamua kuanzisha mfumo huo wa ugharimiaji wa elimu ya juu kupitia Bodi ya Mikopo.

"Ninawapongeza viongozi wetu wa nchi, kwa kuendelea kuweka kipaumbele cha kutenga fedha kwa ajili ya kutoa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu katika awamu zote tangu Bodi hii ilipoanzishwa. Dhamira njema ya Viongozi wetu imewezesha hadi sasa wanafunzi 830,000 kunufaika na mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 8.2 tangu kuanzishwa kwa Bodi", amesema Waziri Mkuu.

Kwa upande wake, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda (MB) amesema kuwa wakati Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani alikuta fedha zinazotolewa kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ilikuwa ni TZS 464 bilioni na na sasa imefikia TZS 787 bilioni.

"Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani bajeti ya mikopo ilikuwa shilingi bilioni 464, aliagiza fedha kwa ajili ya mikopo ziongezwe, na tuliongeza hadi kufikia bilioni 570, tukaendelea hadi shilingi bilioni 654 na sasa ni shilingi bilioni 787", ameeleza Prof. Mkenda.

Kwa upande wake, Rais mstaafu wa awamu ya nne Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete amesema kuwa katika kipindi cha miaka 20, viongozi katika awamu zote wamefanya kazi kubwa katika kuhakikisha Bodi ya Mikopo inajiongezea uwezo ili kuwahudumia vijana wengi zaidi wa Kitanzania.

"Niliyoyaona na kuyasikia yamenifurahisha sana … uongozi ni kazi ya kupokezana kijiti, mwenzako anakimbia mpaka hapa, wewe unapokea unakimbia mpaka pale … nilikabidhiwa na Mzee Mkapa nikafanya nilichoweza, tukaachia awamu ya tano ikafanya ilichokiweza na ikaiachia awamu ya sita … na sasa mambo mazuri zaidi, kazi iendelee", amesema Dkt. Kikwete.

Maadhimisho hayo ya Miaka 20 ya HESLB iliyoanzishwa kwa Sheria mwaka 2004, yalianza tangu tarehe 10 Februari 2025 kwa kutoa huduma kwenye kliniki katika mikoa 7 nchini, lengo likiwa ni kutoa elimu na huduma kwa wadau mbalimbali kuhusu masuala ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Baada ya kliniki hizo, ilifuatia tukio la mbio za hisani tarehe 15 Februari, 2025 zilizoanzia na kuishia katika viwanja vya Farasi jijini Dar es Salaam.

Kilele cha maadhimisho ya miaka 20 ya HESLB kinafanyika kwa siku mbili katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 17 hadi 18 Februari, 2025, kwa kukutanisha wadau wa ndani na nje ya nchi ili kutathmini na kujadili mambo ya kimkakati kuhusu safari ya HESLB ya miaka 20 na maboresho yanayopendekezwa kufanyika ili kuongeza ufanisi zaidi kwa miaka ijayo.

# RAIS SAMIA ANOGESHA MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE

## *Azungumzia ongezeko la bajeti mikopo ya wanafunzi elimu ya juu*



***Arusha, Machi 8, 2025***

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amehitimisha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa ngazi ya kitaifa na kuelezea jinsi serikali ilivyowekeza kwenye elimu kuanzia elimu ya msingi hadi chuo kikuu ambapo amegusia kuhusu ongezeko la bajeti ya mikopo toka mwaka 2021/2022 hadi 2024/2025.

"Bajeti ya mikopo imeongezeka toka TZS 450 bilioni kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 hadi kufikia TZS 787 bilioni kwa mwaka huu wa 2024/2025. Kwa sasa pia serikali inatoa mikopo kwa ngazi ya stashahada … na katika kuongeza hamasa kwenye masomo ya sayansi, tumeanzisha Samia Scholarship kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo ya Sayansi kwenye mitihani ya kidato cha Sita. Vilevile, tumejenga Shule maalumu za Sayansi kwa ajili ya watoto wa kike … na hadi sasa kuna shule angalau moja kwa kila mkoa".

Katika hatua nyingine, Rais Samia amesisitiza kuwa na serikali inayozingatia usawa wa kijinsia katika sekta zote na akaongeza kuwa, "…Nitaendelea kusisitiza kuwepo na usawa wa kijinsia katika sekta zote nchini," amesisitiza Mhe. Samia.

Akifunga hotuba yake Mhe. Rais Samia ametoa rai kwa wanawake na wanaume kuendelea kushirikiana na kulinda amani na utulivu wa taifa la Tanzania.

Maadhimisho ya kilele cha Siku ya Wanawake Duniani Kitaifa yamefanyika Machi 8, 2025, katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha ambapo Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuwa mgeni rasmi.

Maadhimisho hayo yenye kauli mbiu: "Wanawake na wasichana 2025: Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji", yamepambwa na shamrashamra mbalimbali yakiwemo maonesho ya taasisi za serikali na binafsi yaliyofanyika kwa wiki nzima katika mkoa wa Arusha kwa lengo la kutoa huduma na kuelimisha umma. Watumishi Wanawake kadhaa wa HESLB wameshiriki katika maadhimisho hayo yaliyofanyika jijini Arusha.

## NDANI...




03 HESLB YAZINDUA MAADHIMISHO MIAKA 20 KATIKA VIWANJA VYA NYERERE SQUARE





07 WATUMISHI WAPEWA TUZO YA MIAKA 20 TANGU KUANZISHWA KWA HESLB

## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Dkt. Bill Kiwia

**Katibu**
Amani Kakana

**Mhariri**
Jacqueline Msuya

**Wajumbe**
Veneranda F. Malima
Eline Maronga
Jonathan Nkwabi
Ramadhan Namaru

**Designer**
Abdul K. Msangi
+255 736 190 083

**Mawasiliano**
Jengo la PSSSF,
Barabara ya Makole,
eneo la Uhindini
S.L.P 984, Dodoma

**Simu:**
+255 758 067577
+255 739 067577

**Barua pepe:**
info@heslb.go.tz

**Tovuti:**
www.heslb.go.tz

HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE




# MIAKA 20 YA HESLB: TULIKOTOKA, TULIPO, NA TUNAPOELEKEA

Dar es salaam Januari 02,2025

Nakukaribisha tena katika toleo hili la 17 la Jarida la Mtandao HESLB Yako ili kupata habari na matukio yaliyojiri katika robo ya mwaka iliyoishia Machi 31, 2025. Ni wazi mambo mengi yametokea katika sekta ya elimu hususan katika masuala ya ugharimiaji wa elimu ya juu.

Toleo hili limejikita zaidi katika kuonesha mafanikio ya miaka 20 ya utoaji mikopo pamoja na urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu kwa kutambua kuwa ni sehemu muhimu ya kuhakikisha mfuko wa ugharimiaji wanafunzi wahitaji wanaojiunga na masomo katika ngazi ya elimu ya juu kila mwaka wana uhakika wa kupata mikopo na kukidhi mahitaji yao kulingana na uhitaji wao.

HESLB imekuwa na mchango mkubwa katika kuwezesha upatikanaji wa elimu ya juu nchini kwa vijana wa kitanzania wahitaji wenye sifa katika kipindi cha miaka 20 iliyopita huku ikilenga kutoa tathmini ya uchambuzi wa kina kuhusu safari ya HESLB katika kuonesha Athari Chanya, Ubunifu na Huduma, kwa upande mwingine ikielezea matarajio ya baadaye.

Kwa kifupi, mwaka 2024/2025 ulikuwa wa mafanikio makubwa kwa HESLB na kwa Serikali ya awamu ya sita ambapo kwa sasa urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu unafanyika kwa ufanisi kwa kutumia mifumo ya TEHAMA iliyoboreshwa na kuzingatia miongozo ya kiutendaji.

HESLB inamatajio makubwa kuwa mwaka 2025/2026 utakuwa wa tija kubwa katika nyanja za utendaji kazi sambamba na uwajibikaji na utoaji huduma kwa wateja ikiwa ni mwendelezo wa ufanisi wa mwaka 2024/2025.

Kwa dhati kabisa! nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utashi wake wa kuidhinisha ongezeko la fedha kwa ajili ya kugharimia masomo ya wanafunzi wa elimu ya juu kwa kila mwaka mpya wa fedha. Hii inamaanisha wanafunzi wa Tanzania wana uhakika wa kusoma katika ngazi zote za elimu kwa ufadhili, Shukrani pia kwa usimamizi uliotukuka wa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda Pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa HESLB ikiongozwa na Profesa Hamisi Dihenga, sambamba na usimamizi mzuri wa fedha hizo chini ya Mkurugenzi Mkuu Dkt. Bill Kiwia ambapo hayo yote yamefanya HESLB kuwa imara zaidi.

Kwa muktadha huo huo, Meza ya Mwenyekiti inaungana na juhudi za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwakaribisha wanufaika wote ambao madeni yao yameiva na bado hawajaanza kulipa wajitokeze. HESLB imeweka utaratibu rahisi kuwezesha wanufaika kupata ankara (loan statement) za madeni yao na kulipa kupitia kwenye mifumo iliyounganishwa kwenye tovuti yake www.heslb.go.tz

Mwaka 2024/2025, jumla ya wanafunzi 86,646 wamepangiwa mikopo yenye thamani ya TZS 273.46 bilioni; kati yao wanafunzi wa mwaka wa kwanza ni 79,573 na wanafunzi wa mwaka wa pili na kuendelea waliopangiwa mikopo kwa mara ya kwanza ni 7,073.

> *"HESLB inamatajio makubwa kuwa mwaka 2025/2026 utakuwa wa tija kubwa katika nyanja za utendaji kazi sambamba na uwajibikaji na utoaji huduma kwa wateja ikiwa ni mwendelezo wa ufanisi wa mwaka 2024/2025.*




# HESLB YAZINDUA MAADHIMISHO MIAKA 20 KATIKA VIWANJA VYA NYERERE SQUARE

Dodoma, Februari 10, 2025

Mnamo Februari 10, 2025 HESLB ilizindua rasmi maadhimisho ya miaka 20 tangu kuanzishwa kwake katika Viwanja vya Nyerere Square Jijini Dodoma yakiwa na kauli mbiu isemayo "Miongo miwili ya Athari Chanya, Ubunifu na Huduma" ikilenga kuonesha mafanikio na mchango wa HESLB katika sekta ya elimu ya juu nchini kwa kipindi cha miaka 20 iliyopita.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, alikuwa Mgeni rasmi katika ufunguzi wa maadhimisho hayo ambapo aliongoza hafla iliyohudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta ya elimu nchini wakiwemo Wakuu wa Taasisi, Waajiri kutoka sekta za Umma na binafsi, taasisi za fedha, Wanafunzi pamoja na wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu.

Awali, wakati akitembelea mabanda ya washiriki katika maadhimisho hayo, Prof. Nombo ameitaka HESLB kuhakikisha inaongeza wigo wa uelimishaji na kuwafikia wanafunzi wanaotarajia kuomba mikopo hasa waliopo maeneo ya pembezoni, ili wapate elimu ya taratibu za uombaji mikopo kwa usahihi.

Sambamba na hilo, Prof. Nombo amesisitiza uzalendo katika urejeshaji wa mikopo hususani kwa waajiri na waajiriwa kwa kuhakikisha waajiri wanapeleka majina HESLB kwa wakati ili wanufaika wa mikopo ya wanafunzi waanze kurejesha kwa wakati. Aidha, ametoa rai kwa wanufaika kujifichua wenyewe ili kurahisisha zoezi la urejeshaji wa mikopo.

Uzinduzi wa maonesho na huduma kwa wateja umefanyika sambamba katika maeneo mengine sita nchini yakiwemo Dar es salaam, Zanzibar, Arusha, Mwanza, Mbeya na Mtwara ambapo Februari 13,2025 Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mhe. Anna Athanas Paul alizindua jezi za HESLB Marathon, Aidha hafla ya kufunga maonesho ilifanyika katika Viwanja vya Mnara wa Mapinduzi Zanzibar siku ya Ijumaa, Februari 14, 2025 ambapo Mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Ndugu Khamis Abdulla Said.

Matukio mengine katika maadhimisho ya miongo miwili tangu kuanzishwa kwa HESLB yalikuwa mbio za hisani (HESLB Marathon) zilizofanyika tarehe 15 Februari, 2025 katika viwanja vya Farasi jijini Dar es salaam zikilenga kuchangisha fedha kwa ajili ya kuboresha maabara za shule za sekondari na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa elimu kwa ujumla.

Mkutano wa kilele wa maadhimisho haya uliofanyika tarehe 17 Februari, 2025 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere, Dar es salaam, ambapo viongozi mbalimbali wa Serikali na wadau wa elimu wa ndani na nje ya nchi walihudhuria katika tukio hilo muhimu na la kihistoria liliongozwa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mongoni mwa viongozi mshuhuri, alikuwepo Rais wa awamu ya nne Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete ambaye HESLB ilimtunuku kwa kutambua mchango wake wa uongozi hususan wakati HESLB ikiwa changa.

HESLB ilianzishwa kwa Sheria namba 9 ya mwaka 2004 ili kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji wenye sifa na pia kukusanya mikopo kutoka kwa wanufaika ambao mikopo yao imeiva.

Hadi kufikia mwaka huu 2024/2025, HESLB imeshatoa mikopo kwa wanufaika zaidi ya 830,000 yenye thamani ya TZS 8.2 trilioni na imeimarisha mifumo yake tendaji ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja.

> *"Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, alikuwa Mgeni rasmi katika ufunguzi wa maadhimisho hayo ambapo aliongoza hafla iliyohudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta ya elimu nchini wakiwemo Wakuu wa Taasisi, Waajiri kutoka sekta za Umma na binafsi, taasisi za fedha, Wanafunzi pamoja na wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu.*









# MIAKA 20 YA HESLB NA MBIO ZA HISANI

Dar es salaam, Februari 15, 2025

HESLB imeandaa na kufanikisha mbio za hisani kwa mara ya kwanza Februari 15, 2025 katika viwanja vya Farasi vilivyopo Oysterbay, Jijini Dar es salaam kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 20 tangu kuanzishwa kwake.

Lengo la mbio hizo za hisani ni kuimarisha afya sambamba na kukusanya fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya maabara kwa shule mbili za sekondari (moja ya Zanzibar na nyingine ya Tanzania bara) na kuboresha kituo cha huduma kwa wateja cha HESLB.

Akizungumza katika hotuba yake kwa niaba ya Rais wa Zanzibar na Mwakilishi wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi – Zanzibar) Mhe. Hamza Hassan Juma ameipongeza Bodi ya Mikopo kwa mafanikio makubwa katika kuwezesha vijana wengi wa kitanzania kupata elimu ya juu na kuandaa nguvu kazi ya taifa lenye wataalamu wa fani mbalimbali hapa nchini.

"Serikali kupitia Bodi ya Mikopo, imewezesha vijana takribani laki nane (800,000) kupata elimu ya juu…hivyo basi maadhimisho haya ya miongo miwili ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ni fursa ya kutathmini mafanikio yaliyopatikana na kujipanga kwa ajili ya mafanikio makubwa zaidi katika siku zijazo", amesema waziri Jumaa.

Aidha, amemshauri Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kuendelea kuweka mikakati ya kuongeza vyuo na kampasi za vyuo vikuu vingi kule Zanzibar vitakavyokidhi mahitaji ya vijana ili kuendelea kuimarisha udugu katika nyanja zote za kijamii, kisiasa na kiuchumi kupitia uwezeshaji katika elimu ya juu.


Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. QS. Omary Kipanga (MB) amesema kuwa mwaka 2021/22 wakati Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilikuwa TZS 464 bilioni, ambapo ndani ya miaka minne ya uongozi wake, bajeti imepanda hadi kufikia TZS 787 bilioni.

"Kwa kipekee Mheshimiwa mgeni rasmi, tufikishie shukrani zetu kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Dkt. Hussein Mwinyi kwa kazi hii kubwa ya kupandisha bajeti ya Bodi ya Mikopo kwa zaidi ya asilimia 90. Sisi kama Wizara tunajivunia na tunashukuru viongozi wetu kwa utashi wao wa kuona eneo hili la elimu ni eneo muhimu sana", amesema Mhe. Kipanga.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia alisema kuwa Bodi hiyo ilipoanzishwa mwaka 2004 ilianza na wanafunzi elfu arobaini na nane tu (48,000) ikiwa na bajeti ya TZS 53.1 bilioni na kwamba kadri miaka ilivyokuwa ikisonga mbele ndivyo kiasi cha fedha kilivyokua kikiongezeka.

"Kwa mwaka 2024/2025, shilingi bilioni 787 zimetolewa kwa ajili ya wanafunzi laki mbili na elfu arobaini na tano, mia saba tisini na tisa (245,799), ambapo jumla ya mikopo iliyotolewa na Bodi tangu kuanzishwa kwake ni kiasi cha shilingi trilioni 8.2 ambacho kimeweza kusomesha wanafunzi laki nane na elfu thelathini (830,000) nchi nzima" amesema Dkt. Kiwia.

Maadhimisho ya miaka 20 ya HESLB yenye kauli mbiu inayosema, "Miongo Miwili ya Athari Chanya, Ubunifu na Huduma", yaliyoanza tangu tarehe 10 Februari, 2025 kwenye maeneo mbalimbali nchini, yalifikia kilele chake Februari 17, 2025 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es salaam.




# MAGEUZI YA KIMFUMO KATIKA UTENDAJI KAZI WA HESLB




Dar es salaam, Machi 17, 2025

HESLB inafanya mageuzi ya kimfumo katika utendaji kazi katika kituo cha huduma kwa wateja kwa kuanzisha mfumo mpya wa utoaji huduma ambapo itawezesha na kufanya mitandao ya kijamii kuwa katika uso mmoja wa kompyuta.

Maboresho haya ya huduma kwa wateja yanafanyika ili kuimarisha mifumo ya huduma za kidijitali na kuwafikia wateja kwa urahisi zaidi. Mfumo huu unawezeshwa na kampuni ya FLEX Tanzania ambaoni wabobezi wa utoaji huduma katika vituo vya huduma kwa wateja (call/contact centres)

Watoa huduma wa Flex hutumia 'software' ambazo huunganishwa katika barua pepe, Meseji, WhatsApp, Twitter, Instagram, mtandao X, Telegram, pamoja na Facebook ambapo ina dashibodi inayotoa muhtasari wa kina wa data yenye uwezo wa kuunda ripoti nyingi kwa haraka ili kuwahudumia wateja kwa haraka na kwa ufanisi zaidi.

Mkurugenzi Msaidizi wa Habari, Elimu na Mawasiliano HESLB Amani Kakana ametanabaisha kwamba, ...kuunganishwa kwa huduma hii katika kituo kutawezesha wateja kuwasiliana kupitia mitandao ya kijamii na makundi sogozi ambapo itasaidia kurahisisha utoaji na upataji huduma kwa urahisi na kwa uhakika tofauti na kuwa na mfumo mmoja wa kupiga na kupokea simu pekee ambao kituo cha huduma kwa wateja HESLB kinautumia kwa sasa. Amesema Kakana.

Akizungumza na HESLB Yako, mtaalamu wa masuala ya mifumo Bw. Francis Uromi amesema "Mfumo huu utaunganishwa na wataalamu wabobezi kutoka Flex ambao tayari wameshafunga mfumo kama huu karika ofisi mbalimbali ikiwemo za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Afya, Katiba na Sheria, Ardhi, Kilimo, pamoja na Wizara ya Fedha ambapo kwa kiasi kikubwa imewezesha kurahisisha mawasiliano na kuwezesha masuala ya wateja kushughulikiwa kwa wakati" amesema Uromi.

Mfumo wa Flex utawezesha mawasiliano na utatuzi wa changamoto kwa urahisi zaidi na utajumuisha taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia ambapo italenga kuhamisha simu na ujumbe mfupi ('transfers') kutoka taasisi moja kwenda nyingine ikiwa watapata hoja, maswali au pongezi ambazo hazihusiki moja kwa moja na taasisi hiyo.

Muunganiko wa mfumo huu utawezesha kuimarisha uwazi kwa kurahisisha mawasiliano kati ya HESLB na wateja wake wa makundi sogozi ambapo mawasiliano yatakuwa ya kubadilishana ujumbe zaidi 'chatting' na kupata majibu ya papo kwa hapo kama ilivyo katika simu zetu.

Hatua hii ni sehemu ya mkakati wa HESLB wa kupunguza changamoto za muda mrefu, zikiwemo ucheleweshaji wa mawasiliano na kuhakikisha huduma bora kwa wateja wote, Kuunganishwa kwa mifumo ya mawasiliano katika kituo cha utoaji huduma kwa wateja ni kielelezo cha jinsi teknolojia inavyoweza kuboresha sekta za umma na kupunguza changamoto katika jamii.

Huduma hii itapatikana kwa namba za kituo cha huduma kwa wateja (WhatsApp) 0736 66 55 33 pamoja na huduma ya kupiga simu 0736 66 55 33 pamoja na njia ya ujumbe mfupi, Instagram,Facebook,X,Twitter kwa jina la Heslb-Tanzania.



**Februari 12, 2025, Dodoma:** Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Jamhuri wakisikiliza kwa makini maelekezo ya namna ya kuomba na kurejesha mikopo kutoka kwa Meneja wa Ofisi ya HESLB Dodoma Bi. Octavia Selemani (hayupo pichani) walipotembelea Kituo cha Huduma na Maonesho kuelekea maadhimisho ya miaka 20 ya HESLB katika viwanja vya Nyerere Square jijini humo kuanzia Februari 10 hadi 14, 2025. Maonesho kama hayo yalifanyika pia Dar es salaam (Viwanja vya Biafra), Zanzibar (Mapinduzi Square), Mwanza (viwanja vya Furahisha), Mbeya (Viwanja vya Soko la Uhindini), Arusha (Viwanja vya General Tyre) na Mtwara (Viwanja vya Mashujaa).



**Februari 14, 2025, Dar es salaam:** Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Albert Chalamila (kushoto) akipokea fulana ya mbio za hisani anayokabidhiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia alipomtembelea ofisini kwake. Mbio za hisani (HESLB Marathon) kuadhimisha miaka 20 ya HESLB zilifanyika Februari 15, 2025 katika Viwanja vya Farasi, Oysterbay jijini Dar es salaam.




**Februari 15,2025, Dar es salaam:** Baadhi ya washiriki wa mbio za Hisani HESLB, katika maadhimisho ya miaka 20 ya HESLB.



**Februari 15, 2025, Dar es salaam:** Viongozi mbalimbali wakiongozwa na Mgeni rasmi (wa tatu kushoto) Mhe. Hamza Hassan Juma, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili Wa Rais - Zanzibar (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi) aliyemwakilisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, wakimsikiliza kwa makini mtoa hamasa wa mbio za hisani (HESLB Marathon) kuadhimisha miaka 20 ya HESLB katika viwanja vya Farasi, Oysterbay wakati akitoa maelekezo kwa mpiga kipyenga cha mbio hizo (hayupo pichani).



**Februari 17, 2025,** Dar es salaam: Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete (kulia), Rais wa awamu ya nne akiteta jambo na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kilele cha maadhimisho ya miaka 20 ya HESLB yaliyofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC).




**Februari 17,2025, Dar es salaam:** Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia (katikati) akiwa na baadhi ya watumishi wa HESLB katika kilele cha maadhimisho ya miaka 20 ya HESLB. Kulia kwa Mkurugenzi ni Meneja Urejeshwaji Patrick Shoo. Wengine, wa kwanza kushoto ni Christina Chacha, Afisa Mikopo Mwandamizi, wa pili kulia ni Matrona Sway, Afisa Mikopo Mwandamizi akifuatiwa na Imelda Waigama, Afisa Mwanasheria.



**Februari 17, 2025, Dar es salaam:** Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Tanzania akisalimiana na viongozi mbalimbali wa serikali katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC). Mhe. Majaliwa alikuwa Mgeni rasmi katika kilele cha Maadhimisho ya miaka 20 ya HESLB.




**Februari 17, 2025, Dar es salaam:** Mhe. Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akionesha tuzo aliyoipokea kwa niaba ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutambua mchango wa Mhe. Rais Samia katika kuboresha ugharimiaji wa elimu ya juu na vyuo vya kati nchini Tanzania. Tuzo hiyo ilitolewa kwenye kilele cha Maadhimisho ya miaka 20 ya HESLB katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC).



**Machi 08, 2025, Arusha:** Baadhi ya watumishi wanawake wa HESLB katika picha ya pamoja kwenye maadhimisho ya kitaifa ya siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sheikh Amri Abeid ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.




# MLIMBWENDE ATEMBELEA BANDA LA HESLB KATIKA MAADHIMISHO YA MIAKA 20

Dodoma, Februari

'Miss Dodoma University', Dia Musese, ametembelea banda la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) katika maonesho ya maadhimisho ya miaka 20 ya taasisi hiyo yaliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square ambapo alipata fursa ya kujifunza kuhusu historia, mafanikio na huduma mbalimbali zinazotolewa na HESLB kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Dia alizungumza na maafisa wa HESLB na kupata ufafanuzi kuhusu maboresho yaliyofanyika katika utoaji wa mikopo, mfumo wa urejeshaji mikopo, na mpango wa taasisi hiyo kwa miaka ijayo na alisisitiza umuhimu wa HESLB katika kusaidia vijana wa Kitanzania kupata elimu ya juu, huku akitoa pongezi kwa juhudi zinazofanywa ili kuhakikisha wanafunzi wanapata mikopo kwa wakati kuwawezesha kuendeleza elimu yao bila changamoto za kifedha.

"Binafsi najivunia kuwa kati ya wanafunzi wanaosomeshwa na HESLB, kipekee kabisa naishukuru serikali ya Tanzania kwa juhudi zinazofanywa kupitia Bodi ya Mikopo na kuhakikisha vijana tunatimiza ndoto zetu za kielimu ili kujenga taifa imara hapo baadae", alisema Dia.

Ziara ya Dia ambaye ni mtoto wa kwanza katika familia ya mzee Musese na mwanafunzi wa mwaka wa tatu katika Chuo Kikuu Dodoma (UDOM) katika fani ya Sayansi ya Kompyuta; ilivutia washiriki wengi wa maonesho, huku wakionesha shauku ya kujifunza zaidi kuhusu huduma zinazotolewa na HESLB. Dia alitoa wito kwa vijana kuzingatia usomaji wa miongozo ya utoaji mikopo inayotolewa kila mwaka kwa lengo la kuhakikisha kila mhitaji anapata fursa ya kusoma bila kikwazo cha kutokupata mkopo.

Maonesho hayo yalikuwa ni sehemu ya maadhimisho ya Miaka 20 ya HESLB yakilenga kuelimisha umma kuhusu huduma zinazotolewa kwa kutanabaisha historia, mafanikio, na changamoto zinavyotatuliwa, sambamba na mwelekeo wa taasisi katika kuboresha zaidi huduma kwa wanafunzi.



# HESLB na TASAF wamenifungulia Dunia

Dodoma
Zawadi Godfrey Mapogo ni binti mwenye shukrani nyingi kwa fursa alizopata maishani. Anatambua kuwa bila HESLB ndoto yake ya kimasomo ingeishia njiani na huenda angepotea kabisa katika dira ya maisha.

Zawadi anatanabaisha zaidi kwamba, utulivu wa kimasomo awapo darasani unachagizwa na kuwa mnufaika wa mkopo wa elimu ya juu kupitia HESLB, ambapo anakiri kupokea fedha za mkopo wa masomo zinazomwezesha kumudu mahitaji mbalimbali na hivyo kumpatia utulivu wa nafsi pindi awapo darasani.

"Mimi na familia yangu kwa ujumla tunaishukuru sana serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunitoa gizani … mpaka sasa naiona asubuhi njema mbele yangu! Kama siyo HESLB, nisingeweza kumudu gharama za masomo yangu." anasema Zawadi.

Sambamba na hilo anaishukuru Taasisi ya Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa namna ilivyofungua njia katika maisha ya familia yake kwa kuhakikisha wanapata mahitaji yote muhimu hususani ya kielimu kuanzia ngazi ya shule ya msingi mpaka sekondari pamoja na huduma za afya.

"Ninaishukuru HESLB kwa kupitia nyaraka zangu za mkopo nakuridhia kupatiwa mkopo wa masomo kwa asilimia 100….anasema kwa furaha. Niliposoma mwongozo wa mkopo, niliuelewa vizuri na nikahakikisha naweka viambatisho vyote muhimu vya kuonyesha hali ya wazazi wangu ya Uchumi", Anasema Zawadi.

Leo hii, Zawadi anasonga mbele katika safari yake ya elimu akiwa na matumaini makubwa ya kufanikisha ndoto zake na kubadilisha maisha yake na ya familia yake kwa ujumla. Anaamini kuwa kupitia elimu, anaweza kuwa chachu ya maendeleo katika jamii yake na taifa kwa ujumla.

Zawadi ni mzaliwa wa tatu na wa mwisho katika familia ya mzee Mapogo, ni mwanafunzi wa mwaka wa kwanza katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) anasoma Shahada ya kwanza ya Elimu ya Watu wazima na Maendeleo ya Jamii. Matumaini yake makubwa yapo katika elimu anayoendelea kuipata na anaamini kupitia elimu hiyo itamfungulia milango ya mafanikio na kumwezesha kubadilisha maisha yake na ya jamii yake kwa ujumla.




# WATUMISHI WAPEWA TUZO YA MIAKA 20 TANGU KUANZISHWA KWA HESLB

Dar es salaam, 17 Februari, 2025

Watumishi 47 wa HESLB wamepatiwa tuzo kwa utumishi wa muda mrefu katika Maadhimisho ya miaka 20 tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo yaliyofanyika jijini Dar es Salaam katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC). Tuzo hizo zilitolewa kwa wafanyakazi kwa kuthamini mchango wao mkubwa katika kuhakikisha malengo ya HESLB yanafanikiwa husus an katika Utoaji na Urejeshaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia, alisisitiza kuwa mafanikio ya taasisi hiyo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na bidii ya wafanyakazi waliopo HESLB na wale waliofanya kazi HESLB lakini kwa sasa wamehamia taasisi nyingine.

"Leo tunawapongeza wale waliokuwa nasi tangu mwanzo, wakifanya kazi kwa weledi, uadilifu, na kujituma kuhakikisha kila mwanafunzi anayestahili anapata mkopo na kila anaedaiwa kupata elimu ya uzalendo ya Urejeshaji," alisema Dkt. Kiwia.

Mmoja wa waliotunukiwa tuzo hiyo, Bi. Marcelina Msuni, ambaye ni Afisa Mikopo Mwandamizi upande wa Urejeshaji wa mikopo Ofisi ya Dar es salaam, alielezea furaha yake kwa kutambuliwa kuwa miongoni mwa watumishi wa awali wa HESLB.

"Ni heshima kubwa kuona mchango wetu unatambuliwa. Tumepitia changamoto nyingi na mabadiliko ya teknolojia tangu enzi za uchambuzi wa makaratasi mpaka uchambuzi kwa kutumia mifum, lakini pamoja na yote dhamira yetu daima ilikuwa kusaidia vijana kupata kuhakikisha inarejeshwa", alisema Msuni.

Tuzo hizi zilitolewa kwa wafanyakazi wa idara na vitengo mbalimbali, na waliahidi kuendelea kuhudumia Taifa kwa uadilifu na kujituma zaidi. Hii ni mara ya kwanza kwa HESLB kutoa tuzo maalumu kutambua mchango wa wafanyakazi wake tangu ilipoanzishwa mwaka 2004.

Hafla hiyo ilihitimishwa kwa hotuba ya Waziri Mkuu ambaye alisisitiza kuwa serikali itaendelea kuunga mkono HESLB ili kuhakikisha kila kijana mwenye sifa anapata fursa ya kusoma bila vikwazo vya kifedha.

# WASILIANA NASI;

## DODOMA
Jengo la PSSSF,
Br. Makole, eneo la Uhindini
S.L.P 984, Dodoma
Simu +255 758 067577
+255 739 06757
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

## ARUSHA
NSSF Jengo la Mafao,
Ghorofa ya Kwanza
S.L.P 2712,Arusha
Simu: 027 2520128
0624 100 011
0739 102 016
Barua Pepe:
arusha@heslb.go.tz

## MWANZA
PSSSF Plaza, ghorofa ya pili Br. Kenyatta
S.L.P 3051, Mwanza
Simu: 028 2506008
0759 819 350
0738 153 661
Barua Pepe:
mwanza@heslb.go.tz

## ZANZIBAR
Jengo la Michenzani Mall,
Eneo la Michenzani
Ghorofa ya Tano
S.L.P 900,Zanzibar,
Simu: 0779 321 424
Barua Pepe:
zanzibar@heslb.go.tz

## HUDUMA KWA WATEJA
PSSSF Twin Tower
Ghorofa ya chini Mtaa wa Misheni
S.L.P 76068, Dar es Salaam
Simu: +255 758 067 577
+255 739 067 577
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

## MBEYA
Jengo la CAG, Ghorofa ya Nne, Br. Mbalizi
S.L.P 319, Mbeya
Simu: 0738 131 310
0738 131 311
Barua Pepe:
mbeya@heslb.go.tz

## MTWARA
NHC Raha Leo Complex,
Ghorofa ya tatu,
Kitalu Na. 217, Block H, Karibu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P: 969, Mtwara.
Simu: +255 733 068 171
Barua Pepe:
mtwara@heslb.go.tz

## DAR ES SALAAM
Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu,
1 Mtaa wa Kilimo,Tazara,
Br. Mandela
S.L.P 76068,15471
Dar Es Salaam
Simu: 0736 665 533
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz